Jiwe la kiroho la kujengea No.168

# Kuwa Chini ya Damu

*Waefeso 1:7 ''Katika Yeye huyo damu Yake tunao ukombozi wetu, msamaha wa dhambi sawasawa na wingi wa neeema Yake….''*

Sikiliza kile nabii wa Mungu alichosema juu ya hilo**:**

Jambo moja pekee unalopaswa kufanya ni kukubali kile alichokufanyia wewe**.**Hilo tu.Nawe uko chini ya Damu,kila mmoja wenu, vinginevyo Mungu angeharibu/angeangamiza kitu chote**.**Bado uko chini ya Damu ili mradi iko sadaka yenye Damu iliyolala pale kwa ajili ya dhambi zetu. Na siku moja ukiondoka hapa duniani bila kuikubali hiyo sadaka,hapo sasa unasimama kwa dhambi zako mwenyewe (1Yohana 2:2).Na utakuwa aliye hukumiwa tayari, kwa hiyo huwezi kusimama(Yoh 3:16-18)

Mungu ametengeneza njia nzuri hivyo.Unaona, Imani inakuja kwa kusikia(Warumi10:17).Hubiri uponyaji wa kiungu uamini huo, ukubali huo.

Sasa,kila mmoja anajua wanadamu hawawezi kufanya mambo haya.Ni jambo lisilo wezekana. Unaona? Na inapaswa iwe ni Roho wa Mungu.Jambo moja pekee ambalo tunaweza kufanya ni kuwaombea wagonjwa. Siwezi kumponya mtu yoyote, kwa sababu tayari amesha ponywa.Kama mtu yoyote akikwambia kuwa anaweza kukuponya,hilo ni kosa.Unaona?Kama mtu yoyote akikwambia kwamba naweza kukuokoa, hilo ni kosa. kwa vyovyote ninyi nyote mmekombolewa.unaona?

Jambo moja pekee upaswalo kulifanya ni kulikubali hilo.Unakubali kile Yesu alicho kufanyia wewe.alijeruhiwa kwa makosa yako.Kwa kupigwa kwake sisi tumeponywa(Isaya53:4-5) ulikwisha kuponywa; Hilo tayari ni jambo lililopita (1Petro2:24). [1]

Angalia,mifano hii, (mwanamwali mpumbavu) sababu inayowafanya wafe,wapitie utakaso kwa majaribu ya dhiki kuu: Kwa sababu hawako hasa chini ya Damu.Wanadai wako chini ya Damu



lakini hawako.Wataendaje kwenye majaribu ya kuwasafisha wao na ile Damu itakasayo ya Yesu Kristo inaondoa kila dalili ya dhambi na vinginevyo mbali na wewe(1Yohana1:9);Na tayari umekufa, na maisha yako yamefichwa ndani Yake kupitia Mungu na yakatiwa muhuri pale kwa Roho Mtakatifu(Kolosai 3:1-3) Unaenda kuhukumiwa kwa sababu gani?unaenda kutakasiwa wapi? Utasafiwa kitu gani wakati unaonekana ni Mtakatifu ndani ya Kristo,huna dhambi?(Waebrania10:14).Hukumu ni kwa ajili ya nini?Lakini ni hili kundi la waliolala wasioweza kufikia hapo. [2]

Waisrael katika Agano la kale,mahali pekee ambapo Mungu aliweza kukutana nao ilikuwa ni chini ya damu iliyomwagika,walikuja kutoka sehemu mbalimbali za Nchi hiyo mahali alipochinjwa mwana Kondoo,lakini Mungu alikutana nao tu chini ya damu iliyomwagika**.**Chini ya damu ya mwana kondoo ndipo mahali Mungu anapokutana nao. Hapo ndipo anapokutana na watu wake.hapo ndipo anapokutana na kanisa lake**:** Hapo ndipo anapokutana na mahitaji yako,ni chini ya Damu.na nje ya hapo kwenye Damu,hakuna ondoleo au hakuna kusikiwa,ila kupitia Damu tu. (Kutoka 24:1-8 ,Waebrania 9:15-22) [3]

Kwa nini walisema watu wote lazima kuabudia Yerusalemu? kwa maana kuna mahali pamoja tu ambapo Mungu atafanya ushirika na watu;hapo ni chini ya Damu ya sadaka(Kutoka16:1-8). Hiyo ndio sababu ilibidi waje Yerusalemu. Mungu hatakutana na mtu mahali pengine popote, ila chini ya Damu. Unapoikataa Damu, hapo sasa mahali pako pa kukutana na Mungu patakuwa pameondolewa. Mungu alifanya uwamuzi wake wa kwanza pale bustani ya Edeni, kwamba mwanadamu atamwabudu Yeye tu chini ya Damu ya sadaka (mwanzo 3:21)0. Na hapo ndipo mahali pekee ambapo Mungu alikutana na watu kwa wakati huo; na hapo ndipo mahali pekee Mungu aliwahi kukutana na watu/wanadamu; na hapo ndipo mahali pekee anapokutana na watu leo, ni chini ya Damu iliyomwagika ya sadaka (waebrania10:10-14). [4]

Sasa, Israeli, walipokuja kwenye ushirika na Mungu, kulikuwa na mahali pamoja tu pa ushirika na Mungu, na hapo palikuwa maskanini. Katika ile maskani ndipo ambapo sadaka iliyotoka damu ilikuwa nì kitu kisicho na hatia kifunike/kichukue mahali pa chenye hatia,

mwenye dhambi aliyetubu: Ni damu tu.

Sasa, angalia, kwa haraka. Israeli walienda kwenye lile jengo; walimwaga Damu. Na ndani ya hili jengo ilikuwa ni mahali pekee ambapo Mungu angekutana nao na kuwa na ushirika na mwaminio. Ni katika hili jengo ndipo palipokuwa na damu iliyo mwagika. Mwanakondoo alikufa madhabahuni, kila siku. Damu llienda, na moshi mweusi ulining'inia juu ya maskani. Na Mungu asingeweza kuona dhambi, kwa hiyo watu walienda chini ya Damu na wakawa na ushirika{2nyak:6-7}. [5]

Sijali kama wewe ni mmethodist, mbaptist, mpresbiterian, kama mnaweza kusahau tofauti zenu {wakatoliki wa kirumi, na chochote ulicho} na kuja chini ya Damu iliyomwagika, Mungu atakutana na sisi sote pale. Hapo ndipo tunapoweza kukutana sisi sote na kuwa na ushirika katika msingi mmoja. Lakini vinginevyo hatakutana nawe eti kwa sababu ni mmethodist. Hatakutana nawe eti kwa sababu ni mpentekoste. Atakutana nawe chini ya sharti moja tu; hapo ni chini ya Damu. Wakati dhambi zako zimetubiwa {1Yohana1:9}na zimehamishwa uweponi pake. Ni kwa Damu……….Na Damu siku zote iko mbele Yake na kwa hiyo, Anaweza kukuona wewe tu kupitia ile ile Damu iliyomwagika. Na wewe ni mweupe kama theluji unapokuwa umetubu dhambi zako(Isaya1:18)vinginevyo, huko hapo. Huwezi kuwa na ushirika. [4]

Tunakuja mahali ambapo tunatambua kuwa tumetengana. Tumetengwa mbali na Mungu. Na tunakuja katika msingi wa Damu iliyomwagika ya Yesu Kristo. Chini ya hiyo Damu,hapo ndipo mmethodist, mbaptisti, mlutheri, mpresbitierian, mpentekoste wanaweza wote kukutanika kwa msingi wa pamoja, bila kujali mila au Kanuni. Wote wanaweza kukusanyika pale chini ya msingi mmoja na huo ni juu ya Damu ya Yesu Kristo.

Mpaka kanisa lirudi nyuma mpaka mahali fulani, na mbali na mambo ya kienyeji/mila. Lirudi lije kwenye Mpango wa kwanza wa Mungu. Kwamba watu wazaliwe kwenye Ufalme wa Mungu na sio waunganishwe na kanisa.........Hapo sasa ndio wakati ambao ushirika utatawala kila mahali, na Roho wa Mungu ataifunika dunia kamavile maji yafunikavyo bahari, itakapofika mahali ambapo watu wanaweza



kusahau tofauti zao na kuja pamoja katika ushirika chini ya Damu.

Sisi sote hatuwezi kuja chini ya kanuni za kibaptisti au kipresbiterian, chini ya kanuni za kimethodist, chini ya kanuni za pentecoste.Lakini wote tunaweza kukutana na kuwa na ushirika chini ya Damu ya Yesu Kristo kwa sababu ni mpango wa kwanza wa Mungu. Hivyo ni sawa,Amen. Msamaha upo hapo. [6]

Lakini kuna mahali pamoja ambapo tuna vitu ambavyo ni shirika.Chini ya Damu ya Yesu Kristo.Hapo ndipo tunavyo vitu vyote shirika. Hiyo ndiyo njia ya Mungu kwa ajili yetu.Kuweza kukutana kwa vyovyote.Na hakuna mahali pengine zaidi Mungu alipoahidi kukutana na wanadamu;ni chini ya damu iliyomwagika. [7]

Hiyo ndiyo sababu huoni vitu vikifanyika katika makanisa; wanakiri kwamba wanaamini Damu, lakini wanakataa mpango wenyewe wa kuwa peleka /kuwafikisha penye damu, Lile Neno unaona? Kuna njia moja tu, Mungu ataliheshimu lile Neno. Kamwe hataliheshimu lile neno, uje na kusema mimi ni Mromani katoliki; nataka hiki kifanyike "huwezi kufanya hivyo. Methodist,Mbaptist au Mpentekoste,huwezi kufanya hivyo njia pekee uwezayo kufanya ni kuwa chini ya huruma za Mungu kupitia neema yake,ni kuja kupitia Damu iliyo mwagika ya Yesu Kristo;kusema,"Bwana, ninaidai ahadi''unaona? Na halafu kama kweli uko chini ya Damu, Mungu analazimika/anawajibika kwenye hilo Neno. Lakini kwanza, lazima uwe chini ya Damu. Unaliona hilo sasa? [4]

Na njia pekee uwezayo kuwa Mkristo ni kwa kuzaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu (1Petro1:22-23). Na hiyo ndio dawa; kuwa chini ya Damu ya Bwana Yesu. Na unapokiri dhambi zako kwa Mungu, na unapata msamaha kutoka kwa Mungu hapo sasa siyo mwenye dhambi yeye aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi (1Yohana 3:9). Kama unafanya hivyo, siyo kwa kukusudia. Mwabudu mara anapotakaswa hana kumbukumbu tena ya dhambi (Waebr10:1-3) kwa mfano, katika Agano la kale damu ya mafahali ya Mbuzi zilifunika dhambi;haikuondoka mbali dhambi.Lakini Damu ya Yesu inaiondolea mbali.Inaitaliki. Haipo tena (Waebr9:6-14;10:11-13). [8]

Na tumejaribisha elimu, tumejaribisha udikteta, tumejaribisha saikolojia, tumejaribisha udhehebu, tumejaribisha kila kitu kuwasukuma kila mtu pamoja, au kumpenda kila mmoja, pamoja na kila kitu kingine.Hakuna mahali penginepo popote pa ushirika ila tu

chini ya Damu,msingi pekee ambapo Mungu atakutana na mtu. [9]

Na,sasa shetani ninakuamuru kwa Damu ya Yesu Kristo,Damu ambayo inatosheleza, kupitia ule uhai uliokuwa katika hiyo Damu, ambao sasa uko mioyoni mwetu, tumebadilishwa kutoka vile tulivyokuwa mwanzoni na kuwa wa Kristo.Mwanzoni tulikuwa wenye shaka,sasa tu waaminio.Dhambi zetu ziko chini ya Damu "yeye akiriye dhambi zake atapata msamaha" tumekiri dhambi zetu,na tumepata msamaha.Dhambi zetu ziko katika bahari ya usahaulifu (Mika 7:18-19). Hatuwezi tena kushtakiwa kwa dhambi. Tumezitubu hizo. Tumetengeneza mambo, na sasa, ule mtengano mkuu uliokuwa kati yetu na Mungu, umeondolewa. Mungu ameweka dhambi katika bahari ya usahaulifu.Hawezi kamwe akatukumbuka sisi kama wenye dhambi tena (Yeremia 31:34b).Sisi sio wenye dhambi tena tu wana na binti za Mungu, na sasa tupo hapa kwa ajili ya ukombozi wa miili yetu (Warumi 7:24,8:23).Na kwa sababu tu waaminio,lile Neno limesema, lile Neno, Lile Neno, Kristo alilotuachia limesema, ishara hizi zitafuatana na hao waaminio "kama wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa,watapata afya"(Marko16:17-18).Na hili tunalo lifanya, kwa imani tunalifanya hilo katika jina la Yesu Kristo. [10]

Hatukuja pamoja kuzungumza juu ya ujumbe.tumekuja pamoja tuingie kwenye ujumbe na ujumbe ni Kristo;Yeye ni Neno hiyo ni kweli tunapaswa kuingia ndani Yake, kuwa chini Yake ndio Bwana, hilo ndilo tupaswalo kufanya.

Ile Damu ilipakwa wakati wa jioni (Kutoka12:7). Hakuwa anawajibika kwa ajili ya watu wowote wasio chini ya damu.Sio hata mmoja; haijalishi alikuwa nani, hakuwa anawajibika. Wote walipaswa kuwa, sio yeye mwenyewe, lakini ilikuwa ni familia yote.Walikuwa salama pale ile ishara ilipowekwa (Kutoka12:1-37). Hatuwezi kujisikia salama mpaka ile ishara imewekwa (Warumi5:8-10).Hiyo ni kweli lazima uje chini ya ishara hii, Roho Mtakatifu wa Mungu na inamdhihirisha Yesu Kristo kwako kwa sababu inakuja na kuishi ndani yako. [11]

Israel waliamriwa kukaa chini ya Damu mpaka amri ya kutembea itolewe "usitoke nje kuiacha!"Mara unapokuwa chini ya hiyo ishara,unatiliwa muhuri pale "usiondoke hapo"walikaa hapo mpaka usiku wa manane uingie na baragumu/tarumbeta ikapigwa na wakati wa baragumu/tarumbeta ikapigwa, zile pembe za zamani za



kondoo zinapoanza kupigwa, kila mmoja alitembea nje kule vyake, akienda kwenye nchi ya ahadi.kadhalika mwanaume au mwanamke ambaye amejanzwa na Roho Mtakatifu,amefungiwa mbali na yu salama na vyote vya kuumiza na hatari(Waefeso 4:30). Maisha yake yote yanaelekeza kile alicho, popote anapotembea, biashara yoyote afanyayo,yoyote atakaye zungumza naye anapokutana na wanawake, anapokutana na washirika wenzake,anapokutana na chochote ,ile ishara imekaa pale Amina! Inapokuja saa ya kufa ,sitaogopa mabaya yote kwa maana Wewe upamoja nami,ile ishara imekaa pale inapokuja kwenye kufufuka atakuwa pale, kwa maana Mungu atamwita yeye katika siku za mwisho.Yesu alisema hivyo! "Nionapo Damu, ile ishara,nitapita juu yako"(Kutoka12:1-13,29-39).Oh! [12]

Ile ishara, ni ishara ni wewe na Kristo kama watu pamoja unaona? Ni Roho Mtakatifu, maisha yake ndani yako akitenda maisha yake kupitia wewe na hiyo ni kwa matajiri, maskini, au kwa yoyoye atakayepokea hiyo. [13]

Nilifikiri, `oh, Mungu wangu, siku moja itakuja sauti/mlipuko kutoka mbinguni, na waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza {1wathes:4:13-18}.Wale watakatifu wa Agano la kale nyuma kule ambao wanangojea hiyo sauti ije na kutoka hapo kwanza na kuingia kwenye ufufuo, wataingia moja kwa moja katika mstari na kwenda mawinguni,miili hii ya kale inayokufa itabadilishwa na kufanyika kama mwili Wake wa utukufu {1kor:15:51-54}. Itakuwa gwaride la namna gani litakapoanza kuelekea mbinguni siku moja katika siku hizi katika wakati ule wa unyakuo ulioko mbele, oh, tukionyesha Damu ya Yesu Kristo kwa fahari katika vifua vyetu ujumbe wa Mungu wa saa waliyoishi. Hiyo ndiyo saa tunayoitarajia mbeleni ndugu. [14]

Agano jipya ni agano jipya, maisha mapya. Yanamuonyesha Yesu amekamilisha kila alichotakiwa na Mungu kwa ajili yetu kutufanya wana na binti za Mungu wa kweli, tukiwa chini ya Damu hakuna tena hukumu.(Warumi 8:1) Sasa basi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, (siyo wale wanao amini hilo), ni wale ambao wako ndani ya Kristo Yesu, ambao hawaenendi kwa kufuata mwili, lakini wakiongozwa na Roho. Na Neno la Mungu ni Roho na Uzima. (Yohana 6:63). [12]

Lakini Mungu ataangalia alama ya Damu, ile ishara. Hiyo ndiyo itakayotuingiza ndani, kwa sababu hakuna kitakachoingia utukufuni bila kuwa chini ya Damu. Alama ya Damu, Kwamba

tumekikubali kile Mungu alichotutendea sisi katika Kristo. Unaona, hakuna tuwezacho kufanya sisi wenyewe kwa nafsi zetu, sisi ni walioshindwa kabisa. Hakuna njia hata. Mtu alipotenda dhambi, alivuka shimo kubwa/genge kati yake na Mungu hakuacha……Hakuna njia tena ya kurudi nyuma. Lakini Mungu aliye mwingi wa rehema (Waefeso 2:4). Alikubali kitu mbadala. Na kitu hicho mbadala kwa ajili yetu leo ni Yesu Kristo. Huyo pekee ndiye ambaye Mungu atamtambua, ile Damu ya Mwanae itakapokuja wakati huo wakati.(Yohana 1:29). [15].

Sasa, kutoka Adamu hadi sasa, mwanadamu amejaribu kuweka vitu vyake vya mbadala. Amejaribu kufanya kwa werevu kitu fulani kizuri zaidi ya Mungu alivyofanya. Na hicho ni kitu cha asili tu cha mwanadamu mtu amejaribu kufanya kitu fulani kionekane bora, kukifanya kionekane tofauti. Anataka kuingiza mawazo yake katika mpango wa Mungu. Na ndio maana tumesimama usiku wa leo tukiwa na mitengano, wakristo wa duniani, kwa mipaka, kwa mipaka ya kidhehebu. Inafanyika hivyo kwa sababu mwanadamu ameingiza mawazo yake katika mpango wa Mungu. Kutoka wakati wa Adamu mpaka sasa, kama nilivyosema imekuwa hivyo.

Adamu alieleleza mawazo anayofikiri mwanadamu pale katika bustani ya Edeni alipojitengenezea mwenyewe majani ya mtini ili akutane na Mungu (Mwanzo 3:7). Ni kitu fulani ambacho alikifanya mwenyewe. Na kutoka majani ya mtini amejaribisha Elimu, Nguvu, Miji, Sanamu, Ustaarabu, Madhehebu. Lakini bado inabaki vilevile. Mungu anawakubali walio wake chini ya Damu. Na hilo tu.

Elimu imeshindwa kabisa. Kadiri tunavyopata Elimu ndivyo tunavyokwenda mbali kutoka mmoja kwa mwingine. Madhehebu yameshindwa kabisa. Tunachora mistari na mipaka, na kila mmoja akijaribu kulifanya hilo dhehebu juu kuliko lingine, na linavunja ushirika. Ustaarabu umeleta tu kuchanganyikiwa. Miji, minara na vyovyote viwavyo vyote vimeshindwa. Na mpango wa Mungu unabakia ule ule: Kuwa chini ya Damu. Hiyo Damu lazima ionekane kwa wazi kuwa kama Damu. Nyuma kule kwa wakati wa Israeli, wakati Israeli walipopaswa kumuuwa mwanakondoo na kuiweka damu katika miimo ya nyumba na katika vizingiti. Mungu alihitaji hilo(kutoka 12:21-28). Na hiyo ishara lazima iwe pale, haijalishi mahali pengine wale watu wangeonyesha kwamba ni Waisraeli walio



tahiriwa.Wangeweza kusema hivyo, "Tunaamini kila Neno alilosema" Lakini halikuondoa hilo. Ilipaswa waonyeshe hiyo ishara ile Damu lazima ionyeshwe. Na hiyo ndio ilivyo usiku wa leo. Naamini kila mkristo lazima aionyeshe Damu ya Yesu Kristo ambayo imewaosha na mambo ya dunia bila kujali**.**

Sasa katika wakati ule, ile ishara ilibidi iwe mlangoni. Ni lazima iwe pale, bila kujali hiyo nyumba ilikuwa ya kidini kiasi gani, hao watu niwakidini kiasi gani, wamewalea vizuri kiasi gani, watoto wao, wanahudhuria vizuri kanisani kiasi gani, wamevionyesha vizuri namna gani vitu alivyosema Mungu, ilikuwa bado ile saa ya mwisho ilionyesha kati ya kifo na uzima, Damu ilibidi ionyeshwe. Na Damu ilionyesha kuwa kitu kisichokuwa na hatia kimechukuwa mahali pa mwabudu. Na ile kemia ya Damu, ile Damu nyekundu yenyewe ilikuwa ni ishara katika mlango kuwa nyumba hii ilikuwa sehemu chini ya Damu. Sasa huo ulikuwa ni mfano tu. [6]

Tunasoma katika 1Korintho12:13, kwamba; "kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa katika mwili mmoja" na huo mwili ni familia, familia ya Mungu. Na hiyo ni nyumba ya Mungu, na nyumba ya Mungu ni jina la Yesu Kristo.

Jina la Bwana ningome imara; wenye haki wamekimbilia na kuwa salama" (Mithali18:10)

Nimechaguwa kuweka Jina langu katika Mlango wa mwabudu wangu (kumbukumbu16:1-8). Kwa maana familia yangu itakusanyika pale chini ya Damu kama ilivyokuwa kule misri; chochote kilichokuwa nje kilikufa. Na pale hakuna mkate uliotiwa chachu (1korintho5:7-8)

Hakuna mchanganyiko wa mathehebu popote. "katika nyumba yangu, watoto wangu, waliozaliwa kwa chembe zangu"--- Amen. Utukufu kwa Mungu; chembe zangu zimo ndani yao.

Nimeweka Neno langu ndani yao. Nitaliandika katika meza za mioyo yao (waebrania 8:10). Hiyo ni familia yangu familia ya mwili wa Yesu Kristo: Hiyo familia" [16]

Hapo ndipo kanisa litakapo kombolewa kikamilifu, wakati vitu vyotevinapokuja chini ya Damu.Dhambi zako zinapokuja chini ya damu, kuvuta kwako, kupiga kamari kwako, kudanganya kwako, kuiba kwako, uongo wako, wakati kila kitu kitakapoletwa chini ya damu, hapo sasa patakuwepo na ukombozi mkamilifu.

(Isaya 1:18. 1Yohana1:6-9). Kama umemkosesha mtu yeyote lisahihishe. Huwezi kulileta hilo chini ya Damu; hali wezi kukaa. Huwezi kulileta. Kitu fulani hakitakuwacha ulifanye hilo. Wakati wewe mwenyewe kwa ukamilifu wote, umeletwa chini ya Damu, kutakuwepo ukombozi mkamilifu. Hapo sasa utakuwepo na uhuru ambao hujawahi kuuona kamwe.(Yohana 8:31-36). Wakati kila kitu kimewekwa chini ya Damu, unaletwa kutiisha kwenye ufalme wa Mungu. Hapo sasa patakuwa na ukombozi halisi. [17]

Na hivyo ndivyo ilivyo na mkristo wa kweli; je ulijua kuwa mkristo halisi hana dhambi yoyote? Daudi alisema, "Heri (Amebarikiwa) mtu yule ambae Mungu hamhesabii dhambi" (Zaburi 32:1-2) Unapokuwa umeoshwa katika damu ya mwanakondoo(siyo kwa kujifanya kuamini, lakini kwa Damu halisi ya mwana kondoo, Mungu hakuhesabii kwa chochote ambacho kinafanyika, kwasababu uko chini ya Damu naye halioni hilo (Yeremia 31:346). Kuna sadaka yenye Damu; kitu pekee awezacho kukiona ndani, ni vile Ulivyokuwa kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. Alipoweka jina lako katika kitabu cha uzima cha mwana kondoo.(Ufunuo13:8). Hivyo ndivyo awezavyo kuangalia kwa sababu umekombolewa na vyote vilivyo wahi kufanyika:

Umeoshwa katika Damu ya Mwanakondoo. Hakuna tabia chafu ndani yako, kwa sababu Damu ya Mwanakondoo imefanya hayo; na Mungu hawezi kukuhesabia dhambi wewe. (2Kor.5:18-19).Baada ya kuwa na toleo kwa ajili ya dhambi, ikiwa imelala pale ikikungojea wewe (Ufunuo5:6-7,1Yoh 2:2)"Vema unasema hilo linanipa uwanja wa kutosha sasa ndugu Branham; naweza kufanya nitakalo"Siku zote na fanya, sikuzote. Lakini mtu anapoweza kuona hasa Yesu alivyo mtendea, na ageuke tena afanye kitu kinyume na yeye, inaonyesha hajampokea Kristo. [18]

Oh Mungu tunaishi katika saa ya kutisha namna gani, oh njoo Bwana yesu, njoo njoo, Bwana, tusafishe sisi kwa Damu. Ondoa uchafu na uovu mbali nasi. Natuishi Bwana. Natuishi chini ya Damu wakati wote tuwe mbele zako. Ni shauku ya mioyo yetu, na maombi yetu ya uaminifu. [19]



Nukuu za kiingereza
[1] Kung'ang'ania (62-0608),Aya.E-16,E-15
[2] Mhuri wa kwanza (63-0318),Aya. 134-4(120)
[3] Msingi wa ushirika (61-0214),Aya. E-42
[4] Lile shitaka (63-0707m),Uk.17-18
[5] Ushirika ni kwa ukombozi (55-0403), Aya. 203-205
[6] Amesamehewa (63-1028), E-23-26; E-45-46
[7] Tumfanyieje Yesu (64-01266); Aya 2
[8] Tuonyeshe Baba (63-0606),Aya E-8/2-E-9
[9] Mhuri wa nne (63-0321),Aya 298-6{137}
[10] Njia moja pekee tuliopewa na Mungu(63-0731),Aya.253
[11] Ile ishara (63-1128E)Aya,119-121
[12] Ile ishara (63-0901M),Aya.123-124/329-330
[13] Kutaharuki (63-0901E),Aya. 14
[14]Unyakuo (65-1204),Aya.178
[15] Ushawishi (63-1130B),Aya. 9
[16] Mahali pekee alipo pachagua Mungu pa kuabudia (65-1128M)Aya, 227-229
[17] Ukombozi mkamilifu (59-0712),Aya 86
[18] Juu ya Mbawa za Huwa (65-1128E),Aya. 50-51
[19] Edeni ya shetani (65-0829)Aya 27

*jiwe la kiroho la kujengea na 168 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69 D – 75328 Schomberg, Germany (+49) 72357613 Fax : (+49) 72353306. www.biblebelievers.de*

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia. (Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi: kiingereza, kiswahili, andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*